



## **MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA**

### **TAARIFA KWA UMMA AJIRA ZA TRA**

Dar es Salaam, 02 Aprili, 2025

Mtakumbuka kwamba Mamlaka ya Mapato Tanzania ilitangaza nafasi za kazi kuanzia tarehe 6 hadi 19 Februari, 2025. Mtakumbuka pia kwamba tarehe 21 Machi, 2025 Mamlaka ilitoa taarifa kwa umma kwamba baada ya kufunga zoezi la kupokea jumla ya maombi 135,027 yalipokelewa. Kati ya maombi hayo, maombi 112,952 yalikidhi vigezo vya kuitwa kwenye usaili wa kuandika. Tarehe 23 Machi, 2025 Mamlaka ilitoa fursa ya siku mbili (24 na 25 Machi, 2025) kwa waomba kazi ambao walidhani walistahili kuitwa kwenye usaili wa kuandika ila hawakuitwa na baada ya kutolewa kwa fursa hiyo jumla ya maombi 71 yalikidhi vigezo na hivyo kufanya jumla ya maombi 113,023 kukidhi vigezo vya kufanya usaili wa kuandika.

Tunapenda kuwataarifu kuwa, katika maombi hayo, wapo waombaji walioomba nafasi zaidi ya moja, ambapo maombi 113,023 yaliyokidhi vigezo vya kufanya usaili wa kuandika yaliombwa na waomba kazi 86,314. Kati yao, waombaji walifanya usaili wa kuandika walikuwa 78,544 ambao ni sawa na asilimia 91. Waombaji 7,770 ambao ni sawa na asilimia 9 hawakushiriki kwenye usaili kutokana na sababu mbalimbali.

Kama tulivyowataarifu hapo awali kuwa zoezi hili la usaili linafanywa na Mshauri Elekezi ambaye ni Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA). Mshauri huyu alipatikana kupitia mchakato wa manunuzi kufuatia historia na uzoefu wake katika kuendesha masuala ya mitihani kwa weledi na uadilifu. Hivyo NBAA wanaendesha zoezi la usaili katika hatua zote mpaka waajiriwa watakapopatikana. Mamlaka ya Mapato Tanzania haihusiki na kutunga, kuratibu na kusahihisha mitihani ya usaili huo, hivyo itaendelea kubaki kama Msimamizi wa zoezi hili tu.

Kutokana na mpango kazi uliopitishwa, matokeo ya usaili wa maandishi yanatarajiwaa kuwasilishwa na Mshauri Elekezi (NBAA) tarehe 23 Aprili, 2025 na yatatangazwa tarehe **25 Aprili, 2025** kupitia tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Usaili wa vitendo kwa nafasi za Madereva na Waandishi Waendesha Ofisi unatarajiwa kufanyika kwa siku tatu kuanzia **tarehe 2 hadi 4 Mei, 2025** ambao utafuatiwa na usaili wa mahojiano unaotegemea kufanyika kwa siku tatu kuanzia **tarehe 7 hadi 9 Mei, 2025**. Baada ya Mshauri Elekezi kuwasilisha matokeo ya usaili wa mahojiano watakaofanikiwa kushinda usaili huo wataarifiwa **tarehe 18 Mei, 2025** na watatakiwa kuanza mafunzo elekezi **tarehe 22 Mei, 2025 hadi Tarehe 2 Juni, 2025** ambapo wataajiriwa na kuanza kazi rasmi. Ikumbukwe kwamba, mabadiliko yoyote katika mpango huu wa awali, umma utajulishwa.

Sera ya Mamlaka ya Mapato Tanzania ni ajira sawa kwa wote (Equal Opportunity Employer) anayezingatia sifa na vigezo vya muomba kazi. Hadi sasa Sera hii imeteklezwa na inaonekana kuitia idadi ya waombaji walioitwa kwenye usaili wa kuandika. Katika kuhakikisha waombaji wote wanafikiwa kuwa ukaribu, Mamlaka iliendesha usaili wa kuandika katika mikoa nane na Zanzibar kama ifuatavyo:-

1. Dar es Salaam ambayo ilihuisha waombaji kutoka Dar es Salaam na Pwani;
2. Arusha ambayo ilihuisha waombaji kutoka Arusha, Manyara, Kilimanjaro na Tanga;
3. Dodoma ambayo ilihuisha waombaji kutoka Morogoro, Dodoma, Singida, Iringa na Tabora;
4. Mtwara ambayo ilihuisha waombaji kutoka Mtwara, Lindi na Ruvuma;
5. Mbeya ambayo ilihuisha waombaji kutoka Mbeya, Njombe ,Songwe na Rukwa;
6. Mwanza ambayo ilihuisha waombaji kutoka Mwanza, Shinyanga, Mara na Simiyu;
7. Kagera ambayo ilihuisha waombaji kutoka Kagera na Geita;
8. Kigoma ambayo ilihuisha waombaji kutoka Kigoma na Katavi; na,
9. Zanzibar ambayo ilihuisha waombaji Kutoka Unguja na Pemba.

Mtanzania ye yeyote mwenye sifa na vigezo vinavyotakiwa ana nafasi ya kuajiriwa katika Mamlaka ya Mapato Tanzania bila kujali ni mtoto wa maskini, tajiri, kiongozi au mtumishi wa Umma. Tunawahakikisha waombaji wote kuwa Mamlaka **ITASIMAMIA NA KUHAKIKISHA HAKI INATENDEKA** katika zoezi zima ili kupata waajiriwa wanaostahili kwa mujibu wa vigezo vilivywewekwa.

Mamlaka ya Mapato Tanzania inashukuru kwa mrejesho iliyopata kuitia njia mbalimbali ikiwemo mitando ya kijamii kuhusiana na zoezi hili la ajira na inawahakikisha kwamba taarifa zilizopatikana zinafanyiwa kazi na ikidhibitika kwamba zina ukweli wowote, Mamlaka itachukua hatua kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.

Tunawaomba wale wote wenye nia njema na maendeleo ya nchi yetu kuendelea kutoa taarifa zinazoelekea kuharibu zoezi hili kuitia njia mbalimbali zikiwemo;

**TRA Sikika App**

**Simu ya bure: 0800 750 075 / 0800 780 078/ 0800110016**

**Whatsapp: 0744 23 33 33**

**Email: huduma@tra.go.tz / services@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Imetolewa na:

**MOSHI J. KABENGWE**

**Kny: KAMISHNA MKUU**

